CHAPISHO LA UKWELI #4

COVID-19: TAREHE 20 - 26 JULY 2020

TAKWIMU

AFRIKA KUSINI

MAAMBUKIZI YALIYOTHIBITISHWA	471,123
WALIOPONA	297,967
VIFO	7,497

JAMHURI KIDEMOKRASIA YA KONGO

MAAMBUKIZI YALIYOTHIBITISHWA	9,010
WALIOPONA	6,437
VIFO	215

ZAMBIA

MAAMBUKIZI YALIYOTHIBITISHWA	5,249
WALIOPONA	3,285
VIFO	146

IVORY COAST

MAAMBUKIZI YALIYOTHIBITISHWA	15,813
WALIOPONA	10,793
VIFO	99

TANZANIA

MAAMBUKIZI YALIYOTHIBITISHWA	509
WALIOPONA	183
VIFO	21

Source: strategix.co.za

JE, WAJUA?

Ili kujizoesha kunawa mikono kwa kutumia sabuni (yaani Hand Washing With Soap, au HWWS) katika nyakati ngumu, watu wanahitaji kuwa na upatikanaji unaoweza kutegemewa wa maji na uwepo wa sabuni mara kwa mara, na pia ujuzi na motisha ya kuendeleza zoezi hilo. Theluthi moja ya watoto nchini Afrika Kusini wanaishi katika kaya ambazo hazina maji ya bomba nyumbani. UNICEF Afrika Kusini inawahimiza vijana kujihusisha moja kwa moja kupambana na COVID-19 kwa kujitengenezea 'Tippy Taps' katika maeneo hayo ambayo upatikanaji wa maji na sabuni ya kunawa mikono ni mdogo. Bomba za 'Tippy Tap' ni rahisi kutengeneza na zinaweza kutumika popote watu wanapohitaji kunawa mikono yao. Saidia kufanya tabia ya kunawa mikono iwe mazoea kwa kujiunga na #TippyTapChallenge na ujitengenezee bomba lako mwenyewe la 'Tippy Tap.' Ili kupata kuzawadi toka @ZltoRewards na kupata uzoefu wa Tippy Tap yako, tembelea: http://unicef.zlto.co.za. Unaweza pia kuwapa changamoto hii marafiki zako kuunda bomba lao la Tippy Tap, na kila unapoandaa picha na video zako, usisahau kutumia hashtag ya #TippyTapChallenge na #UNICEFSouthAfrica.

Chanzo: UNICEF/ Zlto

SAUTI ZA VIJANA

KHANYA DWEBA (COSAT) - SOUTH AFRICA

SWALI: *"Je, mtu anaweza kuambukizwa kwa kugusa masikio, kwa sababu pia ni eneo la wazi, ingawa halitajwi kamwe?"*

JIBU: Tafiti tofauti zinaonyesha kwamba kuna uwezekano wa kuambukizwa COVID-19 kupitia macho, lakini uwezekano kupitia masikio haujatambuliwa. Kama ilivyo na pua na mdomo, madaktari wanasema macho pia yanaweza kuwa njia ya kuambukizwa. Kunawa mikono mara kwa mara, kudumisha umbali wa kijamii na kuvaa barakoa ni njia ambazo zinapendekezwa ili kuzuia virusi kuenea. Hali kadhalika, masikio hayaminiwi kuwa njia ya maambukizo ya COVID-19, kulingana na Vituo vya Amerika vya Udhibiti na Kuzuia Magonjwa (U.S. Centers for Disease Control and Prevention, CDC). Ngozi inayozunguka sikio kwa nje inalingana zaidi na ngozi ya kawaida tu, tofauti na tishu zilizo katika mdomo, pua na sehemu kwenye paji la uso (sinuses). Hiyo ngozi ni kizuizi ambacho huifanya iwe vigumu kwa virusi kuingia, kulingana na Dk. Benjamin Bleier wa Massachusetts kutoka kituo cha Macho na Masikio mjini Boston.

Chanzo: CBC News: The National

LIYEMA RAFANI (KQ FM) - AFRIKA KUSINI

SWALI: *"Ni nini kimefanya COVID-19 kuenea kwa kasi zaidi Afrika Kusini kuliko nchi zingine kote barani Afrika?"*

JIBU: Mkuu wa shirika la afya la Amref Afrika, taasisi yenye utaalam wa masuala ya afya, amesema kwamba hivi viwango vya juu vinaweza kuwa vimetokana na upimaji mdogo katika nchi zingine za Kiafrika. Unavyofanya vipimo vichache, basi ni kesi chache tu unazopata, na kwa hivyo idadi ilio nchini SA inaweza kuonekana ikiwa juu. Nchi kumi zina karibu ya 80% ya vipimo vyote vilivyofanywa, nchi hizi ni: Afrika Kusini, Moroko, Ghana, Misiri, Ethiopia, Uganda, Mauritius, Kenya, Nigeria na Rwanda. Kufikia Julai 12, Afrika Kusini ilikuwa imefanya vipimo kama 36 kwa kila watu 1,000, ambapo Nigeria imefikia kufanya tu vipimo 0.9 kwa kila watu 1,000, Ghana 11 na Kenya 4. Kwa nchi zingine za Kiafrika, haiwezi kujulikana kikamilifu hasa kinachotokea kwa sababu ya ukosefu wa 'data' yoyote au uwepo wa 'data' isiyokamilika. Shirika la Afya Duniani (WHO) limeonya kwamba Afrika inaweza kuwa inaelekea kwenye mlipuko mkubwa kuliko vile takwimu za sasa zinavyoonyesha.

Chanzo: BBC News World Africa

PATER CHARLES (HUHESO FM KAHAMA) - TANZANIA

SWALI: *"Rais wa Tanzania alitumia mapaipai na mbuzi kama sampuli ili kupima maambukizi ya korona, na Rais wa Uganda pia alitangaza kwamba watu hawana maambukizi lakini ikagunduliwa kuwa wameambukizwa. Sasa nimechanganyikiwa kuhusu vifaa vya upimaji vinavyotumika kutambua maambukizi ya virusi vya korona, na ninahitaji kujua ukweli wa vipimo hivi."*

JIBU: Kuna aina mbili za vipimo vya COVID-19: vipimo vya virusi na vipimo vya kinga za (antibody). Vipimo vya virusi huweza kutambua ikiwa una maambukizi sasa hivi. Vipimo vya kinga (antibody) lakini haviwezi kuonyesha ikiwa mtu ana maambukizi ya COVID-19 ya sasa kwa sababu kinga zetu za mwili zinaweza kuchukua muda wa wiki 1-3 baada ya maambukizi kuingia mwilini kabla ya kutengeneza chembe za kinga. Ili kujua ikiwa una maabukizi kwa sasa, unahitaji kutumia kipimo cha virusi. Upimaji wa COVID-19 hufanywa kwa kuingiza kifaa cha inchi 6 (swab) ndani ya sehemu ilio katikati ya pua na mdomo (nasopharyngeal swab) kwa muda wa sekunde 15 na kuizungusha humo ndani mara kadhaa. Kisha hurudiwa kwa upande mwingine wa pua ili kuhakikisha kwamba sampuli za kutosha zimekusanywa. Kifaa cha 'swab' kisha huingizwa kwenye chombo na kupelekwa katika maabara ili kupimwa. Kwa kweli, kuna aina moja tu ya kipimo inayoaminika. Na inapatikana tu kutoka katika maabara kwa watu ambao madaktari husema wanahitaji kupimwa.

Chanzo: Centers For Disease Control And Prevention

BEENZU M. MUZYAMBA (PAN AFRICA) - ZAMBIA

SWALI: *"Tumeona kwamba Covid19 imebadilisha jinsi tunavyofanya kazi na tukizingatia ukweli kwamba sio kila mtu anayeweza kupata mtandao, basi tunawezaje kuwafikia wale ambao hawawezi kupata habari tunazotoa?"*

JIBU: Vikundi vyote vya wanahabari vijana vimepokea mafunzo ya jinsi ya kuripoti tokea nyumbani, ili kuendelea kufikisha vipindi vyako kwenye vituo vya redio vilio karibu nawe. Redio bado ina idadi kubwa ya wasikilizaji na hufikia mamilioni ya watu ambao hawafikiwi na mtandao. Uwezo wa redio wa kuelimisha na kufahamisha watu kwa maisha yao ya kila siku, na katika hali za dharura, ni muhimu sana leo kama ilivyokuwa tangu zamani, na labda hata ni zaidi leo. Radio inathibitisha umuhimu wake wakati wa janga hili la Covid-19. Wanafunzi kote ulimwenguni wanasikiliza vituo vya redio ili kupokea masomo yanayorushwa kupitia redio. Ujumbe kuhusu jinsi ya kuzuia kuenea kwa maambukizi umeokoa maisha ya watu wengi tayari.

Chanzo: Lifeline Energy / Children's Radio Foundation

GBALET BIANGNE FRANK NAWA - IVORY COAST

SWALI: *"Kwa nini tunaambiwa kwamba watu wamepona COVID-19, na bado tiba haijapatikana?"*

JIBU: Hakuna tiba ya COVID-19 iliyothibitishwa, lakini watu wengi hupona kikamilifu bila kuhitaji matibabu. Ikiwa unajisikia mgonjwa unapaswa kupumzika, kunywa maji mengi, na kula chakula kizuri. Jitenge katika chumba tofauti na wanafamilia wengine, na utumie choo tofauti ikiwa kuna uwezekano huo. Safisha kote ambapo huguswa mara kwa mara. Ikiwa dalili zako hazijabadilika baada ya siku saba, au ikiwa unahisi ugumu wa kupumua na maumivu yameendelea kwenye kifua chako, unapaswa kupiga simu au kutembelea kituo cha huduma ya afya katika eneo lako mara moja.

Chanzo: Avert.org